TANGAZO LA SERIKALI NA. 175 la tarehe 21/3/2025

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KATIKA MRADI WA UPANUZI WA MTAMBO WA KUZALISHA SARUJI KWA KAMPUNI YA LAKE CEMENT YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa Katika Mradi wa Upanuzi wa Mtambo wa Kuzalisha Saruji wa Kampuni ya Lake Cement ya mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 23 Septemba, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa bidhaa zilizoainishwa katika Jedwali la Amri hii zilizoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa nchini kabla ya kibali kupitia forodha na Kampuni ya Lake Cement kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa mtambo wa kuzalisha saruji unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba msamaha katika Amri hii haujatolewa ikiwa bidhaa zitatumika kwa matumizi mengine au zitahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye

hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 31 Mei, 2026 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Lake Cement na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

________

JEDWALI

________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BIDHAA

| Na. | MAELEZO | KIPIMO | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1. | Surface Miner with attachment accessories in dismantled condition | Set | 1 |
| 2. | Road tractors for semi- trailer/tractors/prime mover 370/390 HP with accessories in dismantled condition | Nos | 20 |
| 3. | Mobile crane QAY180V633, make: Zoom Lion, Capacity 180 Ton | Nos | 1 |
| 4. | Escort Hydra 1342AB (Simpson) in CKD Condition with tools and Manuals | Nos | 1 |
| 5. | Wheel Loader-Backhoe | Nos | 3 |
| 6. | Material Handling Equipment | Nos | 4 |
| 7. | Tractor | Nos | 1 |
| 8. | Bulkers | Nos | 8 |
| 9. | Road Cleaner | Nos | 1 |
| 10. | Dozer | Nos | 1 |
| 11. | Excavator | Nos | 4 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Loader | Nos | 4 |
| 13. | Graders or levelers | Nos | 2 |

Dodoma,
11 Machi, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*